**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA**
**SHULE YA SEKONDARI MTUMBATU**
**S. L. P. 170, KILOSA – MOROGORO**

**NAMBA YA SIMU:** 0713696336 / 0753411009

**KUMB Na. MTSS/ADM/2020/…………**
**JINA LA MWANAFUNZI**

______________________________

S.L.P______________________________

______________________________

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MTUMBATU WILAYA YA KILOSA MWAKA, 2021**

1.Nina furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha KWANZA katika shule hii mwaka 2021 HONGERA NA KARIBU SANA.

Shule ya sekondari Mtumbatu ipo umbali wa ½ kilometa kutoka kituo cha mabasi cha Mtumbatu kwenye barabara kuu inayotoka **Morogoro** kwenda **Dodoma.**

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021** na unatakiwa kuripoti shuleni tarehe hiyo ukiwa na mzazi/mlezi wako, mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/03/2021,** hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wale watakaochelewa au kushindwa kuripoti shuleni ndani ya muda uliotolewa.

FOMU YA AFYA imeambatanishwa, hivyo unatakiwa kabla ya kuja shuleni lazima upimwe afya yako ili kuthibitisha uimara wa afya.

**2.Mambo muhimu ya kuzingatia:**

**2.1. Sare ya shule:**

- **WAVULANA**
  - i. Suruali mbili (2) rangi ya Brown, yenye malinda mawili na upana wa chini ni inchi 17 au sm 43 na iwe na mkunjo.
  - ii. Shati nyeupe mbili (2) za mikono mifupi aina ya TOMATO
  - iii. Tai yenye rangi ya Brown yenye michilizi myeupe au inayofanana na rangi ya suruali.
  - iv. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye gidamu visivyo na visigino virefu.
  - v. Soksi zenye rangi nyeusi jozi mbili (2) zisizo na urembo wowote.
  - vi. Sweta rangi ya Brown
  - vii. Sare ya michezo ni bukta na fulana rangi ya njano.

- **WASICHANA**
  - i. Sketi mbili (2) rangi ya Brown, mshono wa Linda box, urefu kutoka magotini kwenda chini ni inch 9 au sm 23
  - ii. Shati nyeupe mbili (2) za mikono mifupi aina ya TOMATO
  - iii. Tai yenye rangi ya Brown yenye michilizi myeupe au inayofanana na rangi ya sketi.
  - iv. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye gidamu visivyo na visigino virefu (bajaji haziruhusiwi)
  - v. Soksi nyeupe ndefu jozi mbili (2) zisizo na urembo wowote
  - vi. Sweta rangi ya Brown.
  - vii. Sare ya michezo ni sketi ya blue iliyokolea na fulana rangi ya njano.
  - viii. Wanaovaa hijab ifanane na shati la shule isiyo na urembo wowote na iwe ndefu



Scanned with CamScanner

**2.2. Vifaa vya darasani:**

i. English – Kiswahili dictionary (1)
ii. Mkebe wa hesabu mmoja(1) (Mathematical set) **HII NI YA LAZIMA MWANAFUNZI ANAPORIPOTI**
iii. Mkoba wa kubebea madaftari (Sio mfuko mbadala)
iv. Madaftari 10 makubwa (Counter book, Quire 2)
v. Kalamu ya wino, kalamu ya risasi na rula.

**3. Vifaa vya usafi.**

- **WAVULANA**
  i. Jembe lenye mpini (JIPYA)
  iii. Fagio kubwa la chelewa.
- **WASICHANA**
  i. Ndoo kubwa ya plastiki lita ishirini (20)
  ii. Kwanja moja (1)
  iii. Fagio kubwa la chelewa.

**MUHIMU:** Unatakiwa kusoma na kuzielewa Sheria na Kanuni za Shule hii zilizoambatanishwa pamoja na fomu hii, ili uweze kuzifuata kipindi chote utakapokuwa mwanafunzi wa shule hii.

***KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MTUMBATU***

M.M.MPEJIWA

**MKUU WA SHULE**

THE HEADMASTER
MTUMBATU SECONDARY
KILOSA.



Scanned with CamScanner

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PRESIDENT'S OFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A:**

THE HEADMASTER,
MTUMBATU SECONDARY SCHOOL,
P.O BOX 170,
**KILOSA**

..........................................................

..........................................................

..........................................................

**PUPIL'S NAME:** ..............................................................................................................

Please, examine the above named as his/ her physical and mental fitness for a full - time student. The examination should be as indicated below in PART B. In each category or sub – category of which will render the applicant ineligible in case of a defect pregnancy (category iv) will also render a girl student ineligible for studies.

**DATE:**.............................................. **SIGNATURE:**.........................................

THE HEADMASTER
MTUMBATU SECONDARY
KILOSA.

**PART B:**

**RE: MEDICAL CERTIFICATE FORM**

**(To be completed by a government medical officer)**

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/ unfit and mentally fit/unfit for a full time student.

i. **AREA** **REMARKS**

a) Eye sight ...........................................................................
b) Hearing ...........................................................................
c) Speech ...........................................................................
d) Limbs ...........................................................................
e) Venereal diseases ...........................................................................
f) Leprosy ...........................................................................
g) T.B ...........................................................................
h) Epilepsy ...........................................................................
i) Asthmatic case ...........................................................................

ii. Neuroses ..........................................................................................................

iii. Other serious diseases:..........................................................................................

...........................................................................................................................

iv. Pregnancy:..........................................................................................................

...........................................................................................................................

**DATE:**................................................ **STATION:**..............................................

**DESIGNATION:**.................................... **SIGNATURE:** ........................................



Scanned with CamScanner

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA

SHULE YA SEKONDARI MTUMBATU

## 1.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

1.1. *Shule inaendeshwa kwa mujibu wa* **sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978.**

*Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana nchini.*

*Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:*

a) *Heshima kwa viongozi, wafanyakazi wote na wanafunzi wengine ni jambo la lazima.*
b) *Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.*
c) *Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation).*
d) *Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.*
e) *Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.*
f) *Kutunza usafi wa mwili na mazingira.*
g) *Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.*
h) *Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote unaotakiwa*
i) *Ni marufuku kuongea* ***lungha za kienyeji*** *uwapo mazingira ya shule.*

### *1.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule:*

1. *Wizi*
2. *Uasherati au ushoga*
3. *Ubakaji.*
4. *Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocain, mirungi, kubeli, petrol, n.k*
5. *Kupiga au kupigana.*
6. *Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.*
7. *Kudharau alama za taifa (k.v. wimbo wa taifa, bendera ya taifa,n.k)*
8. *Kuoa au kuolewa.*
9. *Kupata, kusababisha, kuharibu au kutoa mimba.*
10. *Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.*
11. *Kukataa adhabu halali kwa makusudi.*
12. *Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi katika mazingira ya shule.*



Scanned with CamScanner